


Fidia—Zawadi Bora Zaidi Kutoka kwa Mungu (Sehemu ya 2)

Inategemea sura ya 5 ya kitabu *Biblia Inafundisha Nini Hasa?* kinachopatikana kwenye Tovuti ya jw.org/sw.

LENGO: Chunguza mambo unayoamini na sababu ya kuamini mambo hayo, chunguza kile ambacho Biblia inafundisha, na uone jinsi unavyoweza kuwaeleza wengine mambo unayoamini.



KIFO CHA YESU KINAWEZA KUATHIRIJE MAISHA YETU?

1 CHUNGUZA MAMBO UNAYOAMINI

Unafikiri watu wengine wangesema nini?

Wewe unaamini nini?

Kwa nini unaamini hivyo?

Fidia inaweza kutuletea faida nyingi.


(Tazama sura ya 5 ya kitabu *Biblia Inafundisha*, fungu la 14–17.)

Soma Wakolosai 1:13, 14 na Waebrania 9:13, 14.

Fidia inatuwekaje huru kutokana na kuhisi hatia kupita kiasi kuhusu dhambi zetu?

Soma Waroma 6:23.

Ni katika maana gani wanadamu waaminifu watafaidika kwa umilele wote kutokana na fidia?



Kama zawadi inavyoweza kukufaidi tu unapoitumia, vivyo hivyo fidia inaweza kutuletea baraka nyingi—ikiwa tu tutaonyesha imani kuielekea

Tunapaswa kuonyesha uthamini wetu kwa fidia.

(Tazama sura ya 5 ya kitabu *Biblia Inafundisha*, fungu la 18-22.)

Soma Yohana 17:3 na 1 Yohana 5:3.

Ikiwa tunathamini fidia, tutachochea kufanya nini?

Soma Yohana 3:16 na Yakobo 2:26.

Je, inatosha tu *kusema* kwamba tunaamini katika dhabihu ya fidia ya Yesu?

Wewe binafsi ungependa kuonyesha uthamini wako kuelekea fidia katika njia zipi?

3

ELEZA MAMBO UNAYOAMINI

MTU AKISEMA . . .

Sioni jinsi ambavyo kifo cha mtu mmoja kilichotokea maelfu ya miaka iliyopita *kinavyoweza* kubadili maisha yangu kwa namna yoyote.

UNAWEZA KUMJIBU HIVI . . .

Watu wengi wangekubaliana na wazo hilo. Lakini ninaamini kwamba kifo cha Yesu *kinaathiri* maisha yetu kwa sababu . . .

Unaweza kumwonyesha mtu huyo andiko gani?

Ukizingatia maoni yake, unaweza kuelezaje andiko hilo kwa njia yenye kusadikisha?

MTU AKISEMA . . .

Tunahitaji tu kumwamini Yesu ili tupate wokovu.

UNAWEZA KUMJIBU HIVI . . .

Nakubaliana nawe kwamba kumwamini Yesu ni muhimu. Hata hivyo, ninasadiki kwamba imani tu haitoshi, mengi zaidi yanahitajiwa kwa sababu . . .

Unaweza kumwonyesha mtu huyo andiko gani?

Ukizingatia maoni yake, unaweza kuelezaje andiko hilo kwa njia yenye kusadikisha?
